KUONEKANA NA KUSIKIKA

Siku ya Kimataifa ya Maombi ya Watoto na Vijana

# MUHTASARI WA MUONGOZO

## NYENZO KWAAJILI YA WATOTO AMBAO HAWAJAANZA SHULE

Tumia hii ndani ya wiki moja au mbili kuelekea Siku ya Kimataifa ya Maombi ya Watoto na Vijana Jumapili ya tarehe 28 Machi 2021. Imekusudiwa kutumiwa na watoto ambao hawajaanza shule ambao umri wao unatofautiana kulingana na nchi yako. Tafadhali jisikie huru kurekebisha nyenzo kulingana na muktadha wako.

## NYENZO ZA WATOTO

Tumia hii katika wiki moja au mbili kuelekea Siku ya Kimataifa ya Maombi ya Watoto na Vijana Jumapili tarehe 28 Machi 2021. Imekusudiwa kutumiwa na watoto wenye umri wa kwenda shule (lakini sio sekondari), haswa katika programu za watoto kanisani, shule ya watoto ya Jumapili, jisikie huru kubadilisha na kutumia nyenzo kulingana na watu / hadhira yako.

## NYENZO YA VIJANA

Tumia hii katika wiki moja au mbili kabla ya Siku ya Kimataifa ya Maombi ya Watoto na Vijana Jumapili tarehe 28 Machi 2021. Imekusudiwa kutumiwa na vijana wenye umri wa kwenda shule ya sekondari (takriban miaka 13-18, ingawa hii inaweza kutofautiana kulingana na nchi yako), hasa ndani ya kikundi kidogo / mafunzo ya Biblia / kikundi cha majadiliano, jisikie huru kubadilisha na kutumia nyenzo kulingana na watu / hadhira yako.

## NYENZO YA WATU WAZIMA

Tumia hii ndani wiki moja au mbili kuelekea Siku ya Kimataifa ya Maombi ya Watoto na Vijana tarehe 28 Machi 2021. Hii imekusudiwa kutumiwa na mtu yeyote aliye na umri mkubwa zaidi ya umri wa mwanafunzi wa sekondari, haswa katika kikundi kidogo / mafunzo ya Biblia / kikundi cha majadiliano, jisikie huru kubadilisha na kutumia nyenzo kulingana na watu / hadhira yako.

## * MWONGOZO WA MIPANGO YA IBADA

Hii inatumiwa na majemedari katika kupanga Siku ya Kimataifa ya Maombi ya Watoto na Vijana Jumapili tarehe 28 Machi 2021. Inajumuisha jinsi ya kufanya maombi katika ibada pamoja na mapendekezo ya kushirikisha watoto na vijana wako katika kupanga na kuendesha ibada.

## UTAFITI WA MIPANGO WA IBADA

Hati hii ina maswali ya kuwasaidia viongozi wako kukusanya maoni kutoka kwa watoto wako na vijana wakati wa kushirikiana nao kupanga ibada yako kwenye Siku ya Kimataifa ya Maombi ya Watoto na Vijana.

** Ibada inaweza kufanyika pia kwa maana ya uhalisia wa 'mkutano' wa Jeshi la Wokovu zaidi.*

KUONEKANA NA KUSIKIKA

Siku ya Kimataifa ya Maombi ya Watoto na Vijana

# MUONGOZO WA MPANGILIO WA IBADA

Jumapili ya tarehe 28 Machi 2021 ni Siku ya Maombi ya Kimataifa kwa Watoto na Vijana, na kaulimbiu ya mwaka huu ni 'Kuonwa na Kusikika'. Kuna msemo, uliotokea Uingereza karne ya 15, kwamba 'watoto wanapaswa kuonekana na si kusikika.' Hata hivyo, tunaamini kwamba vijana wanapaswa kuonekana na kusikilizwa katika makanisa yetu; tunaamini sauti za watoto na vijana ni muhimu kwa uhai wa kanisa na kwamba Mungu anaweza na anazungumza na kufanya kazi kupitia vijana kujenga Ufalme wake kwa njia za kushangaza.

Tunakuhimiza utumie angalau baadhi ya mapendekezo yafuatayo kuhusisha watoto na vijana katika ibada yako katika Jumapili hiyo, na pia katika siku za mbeleni kwaajili ya uhai wa kanisa lako kusonga mbele. Fanya kazi na vijana wako na viongozi wao kupanga hili na hakikisha sauti zao zinasikika kama sehemu ya mchakato huu. Ikiwa inasaidia, tumia hati ya 'Utafiti wa ibada' kama mwongozo wa kukusanya maoni na mapendekezo kutoka kwa watoto na vijana wako

## MAOMBI

Kwa kuwa ni Siku ya Kimataifa ya Maombi ya Watoto na Vijana, ni muhimu kufanya maombi kuwa sehemu ya huduma. Hapa kuna njia tofauti ambazo unaweza kutumia kulifanya hii:

- Elekeza watu wazima katika katika kikao chako waweke duara nyuma ya watoto na vijana wako kuwaombea.
- Kabla ya ibada, zungumza na watoto na vijana katika kikao chako kujadili mahitaji yao. Waulize ni nini wanaona kama changamoto zinazowakabili katika jamii yako. Hizi zinaweza kutajwa wakati wa ibada ili kuombewa. Unaweza kuugawa mkutano katika vikundi vidogo kuwaombea vijana.
- Elekeza watoto na vijana kuandika maombi juu ya maswala yanayowaathiri vijana ambayo wangeweza kuombea katika madabahu wakati wa ibada.
- Ikiwa hauna watoto wowote au vijana katika kikao chako, tumia muda kuombea watoto na vijana katika jamii yako, nchi yako na ulimwengu wote. Fanya utafiti juu ya maswala maalum yanayowakabili vijana katika kila moja ya maeneo haya ambayo watu wangeweza kuombea.

## USHUHUDA

Wape nafasi baadhi ya vijana kueleza kuhusu yale ambayo Mungu amefanya katika maisha yao wakati wa ibada. Ushuhuda unaweza kuwa wa moja kwa moja au uliorekodiwa mapema ikiwa unayo njia ya kufanya hivyo.

## MUZIKI

- Waambie vijana wako wachague nyimbo wanazoweza kuimba kwenye ibada. Ikiwa wana uwezo au wako tayari kufanya hivyo, wangeweza pia kuimba na kuongoza nyimbo za kuabudu.
- Jumuisha nyimbo za kufurahisha, ambazo watoto wanaeza kushiriki pia wapatie vifaa vya msingi (ngoma, chekeche, matari, n.k.) ili wacheze.

## MAONESHO YA SANAA

- Elekeza vijana waigize shairi, kucheza, maigizo, nyimbo, n.k., kuelezea nini maana ya wao kusikia na kuthaminiwa.

## UJUMBE

- Tumia Maandiko, mada na maswali yaliyomo katika nyenzo ya kujifunza ili kuandaa ujumbe unaofaa kwa ibada yako.
- Ikiwa kuna kijana anayetaka, anaeweza kutoa ujumbe. Fanya kazi nao kuandaa ujumbe ikiwa ni muhimu, hakikisha wanahisi wanaungwa mkono na kutiwa moyo.
- Kama sehemu ya ujumbe, watie moyo watu wazima katika kutaniko lako kutafakari jinsi wanavyoweka nafasi kwa vijana kuonekana na kusikika katika maisha yao na katika kanisa lako. Unaweza kuwatia moyo kuwaza njia moja ambayo watajihakikishia kufanya hili vyema kila wakati.

KUONEKANA NA KUSIKIKA

Siku ya Kimataifa ya Maombi ya Watoto na Vijana

# MASOMO YA WATOTO WA SHULE YA AWALI

## LENGO

Lengo la somo hili ni kuwawezesha watoto kutambua kwamba wao ni washiriki kamili katika mwili wa Kristo na kushiriki uzoefu wao kwa Mungu.

## KIINI

### Kutambuliwa na kusikika

Tunaamini kwamba watoto ni viongozi, wanafunzi na waamuzi wa leo. Tunaamini watoto wana ujuzi na utaalam wa kipekee ambao kanisa letu na ulimwengu unahitaji. Tunaamini watoto wanasikia na kutumiwa na Mungu kila siku. Tunaamini kwamba watoto ni washirika hai wa mwili wa kristo na wao ni wamuhimu sana kama wengine.

## MUUNDO

Maelekezo haya yanatoa hadithi na shughuli zitakazosaidia watoto wako wa awali kuelewa kwamba hata katika umri wao wamechaguliwa na Mungu. Hatahivyo maelekezo haya yameandaliwa kwa rahisi sana kwakuwa tunajua kwamba sio watoto wote wa awali wanafanana. Tafadhali chagua kile unachohisi kinaweza kuwa sahihi kwao.

## FUNGU LA BIBLIA

### 1 Wakorintho 12:18-27

## HADITHI

***Viongozi**: Unaweza kutumia vifaa au picha kusaidia watoto wako kujihusisha na hadithi hiyo.*

*Mungu alipoumba watu, aliumba miili yetu na sehemu nyingi tofauti. Aliweka mawazo mengi katika kila sehemu yetu. Mungu alitupa mifupa ili miili yetu iweze kusimama vizuri. Alitupa misuli ili tuweze kutembea. Alifanya macho yetu ili tuone, pua zetu zinuse, ndimi zetu kuonja na masikio yetu kusikia. Hata sehemu za miili yetu ambazo hatuwezi kuona zimetengenezwa na Mungu.*

*Mungu alipoumba watu, alituumba tofauti. Lakini kila mmoja wetu ni maalum. Kama vile zilivyo sehemu nyingi tofauti katika miili yetu, kuna watu wengi tofauti kanisani. Wengine ni watu wazima, wengine ni vijana au watoto, wengine ni wazee sana, na wengine ni watoto wadogo, lakini sisi wote ni maalum kwa Mungu.*

*Hadithi mbadala unazoweza kuchagua kutumia kwa kikundi chako:*

- *Toleo la Biblia ya watoto 1 Wakorintho 12: 18-27.*
- *Wewe ni Maalum kutoka kwa Max Lucado.*
-

## MAMBO YA KUFANYA

### Mabango ya Maombi

Kutumia ufundi wowote au vifaa vya sanaa unavyoweza kuwa navyo, waelekeze watoto kutengeneza bango ambalo linaonyesha kile ambacho wanapenda kuzungumza na Mungu.

### Maombi ya ABC

Kama kikundi, kwa kutumia kila herufi ya alfabeti, taja jambo moja kumshukuru Mungu.

### Sanamu

Waambie watoto watengeneze mchezo au sanamu ya plastiki ya kitu ambacho Mungu anapenda.

KUONEKANA NA KUSIKIKA

Siku ya Kimataifa ya Maombi ya Watoto na Vijana

# MASOMO YA WATOTO

## LENGO

*Lengo la somo hili ni kuwawezesha watoto kutambua kwamba wao ni washiriki kamili katika mwili wa Kristo na kushiriki uzoefu wao kwa Mungu.*

## KIINI

### Kuonekana na kusikika

Tunaamini kwamba watoto ni viongozi, wanafunzi na waamuzi wa leo. Tunaamini watoto wana ujuzi na utaalam wa kipekee ambao kanisa letu na ulimwengu unahitaji. Tunaamini watoto wanasikia na kutumiwa na Mungu kila siku. Tunaamini kwamba watoto ni washirika hai wa mwili wa kristo nan a wao ni muhimu sana kama wengine.

## MUUNDO

Mwongozo huu unatoa hadithi inayoambatana na maswali ya "kujiuliza"  na " majibu", na vile vile 'vidokezo vya kuongea' kuifanya hadithi na wakati wa maswali vijitosheleze. Hadithi na maswali ya kujiuliza yanategemea kanuni za ujifunzaji za uchunguzi. Hii inaweza kuwa mfano wa kutafakari zaidi kuliko kawaida unayotumia katika huduma ya watoto wako.

## KIFUNGU CHA BIBLIA

**1 Wakorintho 12:18 - 27**

## HADITHI

***Viongozi**: Unaweza kutumia vifaa au picha kusaidia watoto wako kujihusisha na hadithi.*

*Mungu alipoumba watu, aliumba miili yetu na sehemu nyingi tofauti. Aliweka mawazo mengi katika kila sehemu yetu. Mungu alitupa mifupa ili miili yetu iweze kusimama vizuri. Alitupa misuli ili tuweze kutembea. Alifanya macho yetu ili tuone, pua zetu zinuse, ndimi zetu kuonja na masikio yetu kusikia.*

*Hata sehemu za miili yetu ambazo hatuwezi kuona zimetengenezwa na Mungu na ni muhimu katika kuafnya miili yetu kufanya kazi, kwa mfano mapafu, tumbo na ubongo wetu.*

*Kuna sehemu za miili yetu ambazo zinatakiwa kufunikwa. Nazo ni muhimu pia, ingawa ni vya faragha / siri.*

*Mungu alipoumba watu, alituumba tofauti. Lakini kila mmoja wetu ni muhimu. Kama vile zilivyo sehemu nyingi tofauti katika miili yetu, kuna sehemu nyingi katika Mwili wa Kristo. Wengine ni watu wazima, wengine ni vijana au watoto, wengine ni wazee sana, na wengine ni watoto wadogo.*

*Wengine tuna ujuzi, tunaweza kuongea au kuimba mbele ya kanisa / kwenye jukwaa. Wengine wana busara na watasaidia wengine kuielewa Biblia. Wengine wana huruma sana na huwajali watu wengine. Wengine ni wakarimu sana na hufanya vitu ambavyo hakuna mtu anayeona, na kurahisisha maisha kwa kila mtu.*

*Kila mmoja wetu, bila kujali umri wake au ni ana vipaji vipi, ana nafasi maalum katika Kanisa. Kila mmoja wetu ni sehemu ya Mwili wa Kristo.*

## MASWALI YA KUJIULIZA

Maswali haya ya mtindo wa kujiuliza yameundwa kusaidia watoto kufikiria kwa kina na kwa kutengeneza picha juu ya Mungu. Huna haja ya kufanaya majadiliano juu ya majibu yao; wape ruhusa tu kuyajibu.

- Najiuliza sehemu gani ya hadithi unaipenda zaidi?
- Najiuliza ni sehemu gani ya hadithi ni muhimu zaidi?
- Najiuliza kama uko mahali fulani ndani ya hadithi hii, au ni sehemu gani ya hadithi inayokuhusu?

- Najiuliza Mungu amekupa ujuzi gani na vipaji vipi?
- Najiuliza ni vipi Mungu anaweza kukutumia leo?
- Najiuliza jinsi Mungu anavyosema nawe?

Baada ya watoto kujibu maswali, waeleze kwamba watapata wakati wa majibu. Wanaweza kuchagua shughuli yoyote iliyopo ili kuunganishwa na Mungu na kuelezea jinsi wanavyohisi juu ya hadithi waliyosikia.

Omba na watoto wakati wakiingia katika  wakati wa majibu; waruhusu watoto kuombeana kwa sauti ikiwa watakua huru kufanya hivyo.

## WAKATI WA MAJIBU

Itakuwa vizuri kuwa na shughuli kadhaa za majibu zinazopatikana kwaajili ya watoto ili waweze kushiriki na Mungu, hata hivyo Roho anawaongoza. Sio watoto wote wanaweza kutumia wakati wao wa majibu kujiunganisha na Mungu, ni sawa - kujisikia tu kuwa na furaha na kuwa salama katika kucheza au kufanya ufundi ndani ya kanisa ni sehemu muhimu ya ukuaji wao wa kiroho.

Njia ambazo watoto wanaweza kuchagua kujibu ni kupitia:

- Rangi, kalamu, penseli ya rangi na karatasi
- Kufinyanga
- Vitabu vya hadithi, kama vile kitabu cha hadithi za Bibilia ikiwa unacho
- Sanamu
- Vitalu vya ujenzi
- Wimbo
- Ngoma
- Mchezo wa kufikirika
- Kuunda na kusimulia hadithi

## POINTI ZA KUZUNGUMZA

- Watie moyo watoto kuzungumza juu ya uzoefu wao na Mungu.
- Wakumbushe kwamba Mungu anawatumia; huwa hasubiri wakue kwanza.
- Ongelea jinsi vipaji vya kila mtu zilivyo muhimu - hakikisha untaja ujuzi na vipaji ambavyo havionekani katika huduma za kanisa.

KUONEKANA NA KUSIKIKA

Siku ya Kimataifa ya Maombi ya Watoto na Vijana

# MASOMO YA VIJANA

## LENGO

***Viongozi**: Lengo la somo hili ni kuonyesha kwamba Mungu hutumia vijana kutimiza malengo yake na kwamba anataka kufanya kazi na kuzungumza kupitia vijana wako!*

## UTANGULIZI

Kuna msemo, uliotokea Uingereza karne ya 15, kwamba, 'watoto wanatakiwa kuonekana na si kusikika' - mtazamo ukiwa ni kwamba watoto hawakuwa na chochote cha thamani cha kutoa au kujadili. Hatahivyo, tunaamini kwamba vijana wanatakiwa kuonekana na kusikika katika makanisa yetu; tunaamini sauti za watoto na vijana ni muhimu kwa uhai wa kanisa na kwamba Mungu anaweza na anazungumza na kufanya kazi kupitia vijana kujenga ufalme wake kwa njia za ajabu.

## SHUGHULI

***Viongozi**: Tumia moja kati ya shughuli zifuatazo au zote mbili, au fikiria njia yako mwenyewe, kuonyesha umuhimu wa kusikilizwa.*

### Lugha ya vitendo:

Gawanya kikundi chako katika timu mbili na uziweke timu hizo katika pande za chumba / uwanja wako. Zipe timu ujumbe ulioandaliwa au wape dakika moja kuandaa ujumbe wao wenyewe. Ujumbe unapaswa kutoa maelekezo, na kazi ya timu nyingine na kutekeleza maelekezo. Timu lazima ziwasiliane bila kuongea, waigize au watamke ujumbe kwa namna fulani (wasifanye au kuonyesha dhahiri kile wanachojaribu kusema). Endapo timu nyingine ikihisi kwamba imeelewa ujumbe, lazima wafanye kwa bidii kitendo walichoambiwa kufanya.

**Ufupisho:**

- Ilikuwa ngumu kiasi gani kuelewa ujumbe unaowasilishwa?
- Ni nini kilifanya iwe changamoto kuelewa?
- Ni nini kingeweza kurahisisha uelewa?
- Je, hii inatufundisha nini kuhusu mawasiliano?

### Wimbo wa Timu:

Gawanya kikundi chako  nusu kwa nusu na uiagize kila timu kutumia dakika moja kutengeneza wimbo. Hii inaweza kuwa kwaajili ya kuwasilisha ujumbe, au kitu kisicho na mpangilio kabisa. Baada ya dakika kuisha, zielekeze timu zote mbili kukabiliana. Hesabu mpaka tatu na timu zote mbili ziimbe kwa kelele kwa kadiri wawezavyo. Baadaye, baadae iulize kila timu ni nini timu nyingine iliimba. Ikiwa hawajui, rudia zoezi kisha uwaulize tena.

**Ufupisho:**

- Ilikuwa ngumu kiasi gani kusikia kile timu nyingine ilikuwa inasema?
- Ni nini kilifanya iwe changamoto kusikia?
- Ni nini kinachoweza kurahisisha usikivu?
- Je, hili linatufundisha nini kuhusu mawasiliano?

## MAJADILIANO

***Viongozi**: Muombe mtu asome vifungu vya Biblia kwa sauti kwenye kikundi. Ikiwa una wakati, unaweza kumuomba mtu mwingine asome tena kutoka kwenye tafsiri tofauti. Tumia maswali yaliyotolewa hapa chini kuhamasisha majadiliano. Jisikie huru kuongeza maswali yako na uliza maswali fuatilizi kulingana na mtiririko wa jinsi watu wanavyoshiriki ili kuendeleza majadiliano.*

Kwanza, tuangalie baadhi ya mifano ya vijana waaminifu waliotumiwa na Mungu kutimiza mapenzi yake:

### Daudi

**Soma 1 Samweli 17**

- Unapata mtazamo gani kutoka katika kifungu hiki?
- Sauli alitoa sababu gani ya kutomtaka Daudi kumkabili Goliati (mst 33)
- Jibu la Daudi lilikua nini (mst 37)
- Tunajifunza nini katika kifungu hiki kuhusu jinsi Mungu anavyofanya kazi? *(Mungu yuko tayari na anao uwezo wa kufanya kazi kupitia vijana – huwa hachagui wale wanaoonekana kuwa na vigezo machoni pa wanadamu)*

### Mariamu

**Soma Luka 1:26-38**

- Unapata mtazamo gani kutoka katika kitabu hiki?
- Mariamu alijibu nini kuhusu habari ya kumzaa Yesu?
- Unafikiri ingekua rahisi kiasi gani kumwamini Mungu kama ungekuwa katika nafasi ya Mariamu?
- Je! Kwa kumchagua Maria, Mungu anatuambia nini kuhusu yeye ni nani? *(Tena, Mungu hutumia wale walio na nguvu na ushawishi kidogo wa kidunia kumfanyia mambo makubwa. Wanatakiwa tu kuwa tayari.)*

### Pollard na Wright

Tarehe 27 Machi 1883, vijana wawili wa Uingereza maafisa wa Jeshi la wokovu, Captain George Pollard na Luteni Edward Wright walifika Port Chalmers, New Zealand. Mwaka 1882 baadhi ya watu wa New Zealand walimwandikia mwanzilishi mwenza wa Jeshi la wokovu, William Booth, wakimuomba awatumie maafisa katika koloni lililokua katikati ya mporomoko wa uchumi. Pollard (miaka 20) na Wright (miaka 19) walitumwa na Jeshi liliwasha moto New Zealand siku ya Jumapili tarehe 1 Aprili 1883. Walifanya mikutano minne katika ukumbi wa Dunedin Temperance na baadae kidogo mikusanyiko ya Jeshi ilijaza watu.

Haraka Pollard alianzisha Jeshi huko Auckland, Christchurch na Wellington, na nyumba za uokoaji zilifunguliwa katika vituo hivi. Kufikia mwisho wa 1884, Jeshi la Wokovu lilikuwa na vikao 30 na zaidi ya maafisa 60 huko New Zealand![1]

Fikiria jinsi hadithi ya Israeli ingeweza kuwa tofauti kama Mfalme Sauli angekataa ombi la Daudi kumkabili Goliati kulingana na umri wake na uzoefu. Je! Kanisa lingekuwepo kama tunavyojua ikiwa Mariamu angepinga mpango wa Mungu kwake au Yusufu angechagua kuachana na kutomuunga mkono Mariamu? Ingekuaje kama William Booth asingewaamini Pollard na Wright, au watu wa New Zealand wangekataa kusikiliza au kuongozwa nao kwa sababu ya umri wao?

- Je! Umewahi kuhisi kutostahili kuchukua jukumu au kwamba sauti yako haina umuhimu kwa sababu wewe ni mdogo sana au hauna sifa, nk?
- Kulingana na mifano tuliyoiangalia, unafikiri ni vipi vigezo vya kumtumikia Mungu na kusema kwa niaba yake?
- Je! Kuna vigezo au vizuizi visivyo vya lazima ambavyo unafikiri kanisa letu, viongozi wetu au sisi wenyewe tunaweka ambavyo vinawazuia watu kumtumikia Mungu kikamilifu?
- Je! Kuna unahisi Mungu anakuita umtumikie kwa njia maalum?
- Je! Kuna chochote kinakuzuia kufanya hivyo?

***Viongozi:** Unaweza kuandika majibu kwa maswali yafuatayo ili kuwasilisha na kujadili na viongozi wako wa kanisa.*

- Je! Unaweza kufikiria njia zozote ambazo familia yako ya kanisa inaweza kukusaidia kumtumikia Mungu kikamilifu na kuchangia kwa maana katika maisha ya kanisa lako?
- Kama ungekuwa unaliandikia kanisa lako barua ukielezea jinsi linavyoweza kukufanya ujisikie unathaminiwa na kusikia zaidi, ungesema nini?

## MUHTASARI

Vijana ni wa thamani kwa Mungu! Mara nyingi hutumia vijana kumsema na kutimiza mapenzi yake wakimwamini na kujitiisha kwake. Mungu anataka kukutumia, kwa hivyo tafuta fursa ya kusema na kutenda kwa kumtii.

## OMBA

***Viongozi**: Omba pamoja na vijana ili kuwapa ujasiri wa kusema kwa ujasiri na kuishi kwa Mungu kwa njia ambazo anawaongoza bila kujali mapungufu yoyote yanayoonekana. Omba kwamba kanisa lako liwe jamii inayowakubali vijana na kutoa nafasi kwa sauti zao kusikika. Mshukuru Mungu kwaajkili ya mahali ambapo hii tayari inafanyika na kwa mahali ambapo Mungu anafanya kazi katika maisha ya vijana wako.*

## MIPANGO YA IBADA

***Viongozi**: Jumapili ya tarehe 28 Machi 2021 ni Siku ya Maombi ya Kimataifa kwaajili ya Watoto na Vijana. Jadili na viongozi wako wa kikao jinsi vijana wanavyoweza kuhusishwa katika ibada na kupewa nafasi ya kusikilizwa kama sehemu ya hili. Ikiwa wanaweza kujumuishwa, unaweza kutumia muda katika kipindi hiki kufanya maandalizi na mipango yoyote muhimu na vijana.*

---

[1] 'The 'Sallies' come to New Zealand', URL: https://nzhistory.govt.nz/page/sallies-come-to-new-zealand, (Ministry for Culture and Heritage), updated 17 May 2017.

## LENGO

***Viongozi:*** *Lengo la somo hili ni kuorodhozesha umuhimu wa kuwa na washiriki hai vijana na watoto kaitka uhai wa kikao/jamii na kuwasaidia ninyi kutafakari jinsi ya kutengeneza nafasi ya wao kushiriki.*

## UTANGULIZI

Kuna msemo, uliotokea Uingereza karne ya 15, kwamba, watoto wanatakiwa kuonekana na si kusikika, - mtazamo ukiwa ni kwamba watoto hawakuwa na chochote cha thamani cha kutoa au kujadili. Hatahivyo, tunaamini kwamba vijana wanatakiwa kuonekana na kusikika katika makanisa yetu; tunaamini sauti za watoto na vijana ni muhimu kwa uhai wa kanisa na kwamba Mungu anaweza na anazungumza na kufanya kazi kupitia vijana kujenga ufalme wake kwa njia za ajabu.

## MAJADILIANO

***Viongozi:*** *Tumia maswali yafuatayo kuhimiza majadiliano. Jisikie huru kuongeza maswali yako na pia uliza maswali fuatilizi kulingana na mtiririko wa jinsi watu wanavyoshiriki ili kuendeleza majadiliano.*

Kwanza tutaangalia baadhi ya mifano ya vijana waaminifu waliotumiwa na Mungu kutim iza mapenzi yake:

### David

Soma historia ya Daudi katika kitabu cha 1Samweli 17

- Sauli alitoa sababu gani ya kutomtaka Daudi kumkabili Goliati (mst 33)
- Jibu la Daudi lilikua nini (mst 37)
- Tunajifunza nini katika kifungu hiki kuhusu jinsi Mungu anavyofanya kazi? *(Mungu yuko tayari na anao uwezo wa kufanya kazi kupitia vijana – huwa hachagui wale wanaoonekana kuwa na vigezo machoni pa wananadamu.)*

### Mary

Soma hadithi ya Mariam kutembelewa na malaika Gabriel kwatika kitabu cha Luka 1:26 – 38 na majibu ya Yusufu kwa habari zake katika Mathayo 1:18 – 24.

- Mariamu alijibu nini kuhusu habari ya kumzaa Yesu?
- Ikiwa ungekuwa Yusufu katika hali hiyo, unafikiri majibu yako yangekuwaje?
- Ingawa Bibilia haisemi umri wake, inaelekea kwamba Mary alikuwa katikati ya ujana wakati Mungu alichagua kumtumia. Je! Hii inafunua nini juu ya Mungu? *(Tena, Mungu hutumia wale walio na nguvu na ushawishi kidogo wa kidunia kumfanyia mambo makubwa. Wanatakiwa tu kuwa tayari.)*

### Pollard na Wright

Tarehe 27 Machi 1883, vijana wawili wa Uingereza maafisa wa Jeshi la wokovu, Captain George Pollard na Luteni Edward Wright walifika Port Chalmers, New Zealand. Mwaka 1882 baadhi ya watu wa New Zealand walimwandikia mwanzilishi mwenza wa Jeshi la wokovu, Willium Booth, wakimuomba awatumie maafisa katika koloni lililokua katikati ya mporomoko wa uchumi. Pollard (miaka 20) na Wright (miaka 19) walitumwa na Jeshi liliwasha moto New Zealand siku ya Jumapili tarehe 1 Aprili 1883. Walifanya mikutano minne katika ukumbi wa Dunedin Temperance na baadae kidogo mikusanyiko ya Jeshi ilijaza watu.

Haraka Pollard alianzisha Jeshi huko Auckland, Christchurch na Wellington, na nyumba za uokoaji zilifunguliwa katika vituo hivi kuu. Kufikia mwisho wa 1884, Jeshi la Wokovu lilikuwa na vikao 30 na zaidi ya maafisa 60 huko New Zealand![1]

[1] 'The 'Sallies' come to New Zealand', URL: https://nzhistory.govt.nz/page/sallies-come-to-new-zealand, (Ministry for Culture and Heritage), updated 17 May 2017.

Fikiria jinsi hadithi ya Israeli ingeweza kuwa tofauti kama Mfalme Sauli angekataa ombi la Daudi kumkabili Goliati kulingana na umri wake na uzoefu. Je! Kanisa lingekuwepo kama tunavyojua ikiwa Mariamu angepinga mpango wa Mungu kwake au Yusufu angechagua kuachana na kutomuunga mkono Mariamu? Ingekuaje kama William Booth asingewaamini Pollard na Wright, au watu wa New Zealand wangekataa kusikiliza au kuongozwa nao kwa sababu ya umri wao?

- Kulingana na mifano tuliyoiangalia, unafikiri mahitaji muhimu ya kumtumikia Mungu na kusema kwa niaba yake ni yapi?
- Je! Unafikiri kuna mahitaji muhimu au vizuizi visivyo vya lazima ambavyo vimewekwa na muundo wa Kanisa, viongozi wake au sisi wenyewe ambavyo inawazuia watu kumtumikia Mungu kikamilifu? Ikiwa ndivyo, ni vipi kati ya hivyo?

1 Wakorintho 12: 12-27 inaelezea Kanisa kama mwili mmoja wenye viungo vingi. Ijapokuwa sehemu hizo ni tofauti na zinatumika kwa malengo tofauti, kifungu hiki kinathibitisha kuwa sehemu zote ni muhimu na zinapaswa kuthaminiwa na kukumbatiwa kama sehemu ya mwili mmoja wa Kristo.

Wazo lingine muhimu la kibiblia ambalo linakubaliwa na Jeshi la Wokovu ni kwamba kanisa ni 'ukuhani wa waumini wote' na Kristo ndiye Kuhani wetu Mkuu.

- Je! Unafikiri picha hizi za Kanisa zinajumuisha watoto na vijana? Kwanini?
- Ikiwa ni hivyo, ni kwa jinsi gani kikao / jamii yako inawakumbatia vijana kikamilifu kama sehemu ya Mwili wa Kristo na ukuhani wa waumini wote?
- Je! Ni mitazamo na vipaji gani vya kipekee ambazo vijana wanachangia katika uhai wa kikao / jamii yako?

Mwandishi na mwanaharakati Arundhati Roy aliwahi kusema, 'Kwa kweli hakuna kitu kama "wasio na sauti". Kuna walionyamazishwa kwa makusudi tu, au ikiwezekana wasiosikika.

- 'Je! kikao/jamii yako hutengenezaje nafasi kwa sauti za vijana kusikika?
- Je! Kuna kitu chochote ambacho kikao / jamii yako hufanya au haifanyi ambacho kinaweza kuwanyamazisha vijana, kwa makusudi?
- Je! Unaweza kufikiria njia yoyote ambayo ya kuboresha eneo hili?
- Je! Wewe binafsi unawezaje kuchangia hili?
- Je! Uko tayari kujitolea faraja, nafasi, ushawishi, n.k., ili vijana wenye ushawishi zaidi waweze kujumuishwa, na wazidi kuonekana na kusikika katika kikao / jamii yako?

## MUHTASARI

Vijana na sauti zao ni wa thamani mbele za Mungu na kwa Kanisa lake! Mara nyingi hutumia vijana kumsema na kutimiza mapenzi yake wakimwamini na kujitiisha kwake. Sisi, kama Kanisa lake, lazima tuwatie moyo na kuwapa nafasi vijana ili sauti zao zisikike wanapomtumikia Mungu kwa njia yao ya kipekee kama washiriki wa thamani wa Mwili wa Kristo.

## OMBA

***Viongozi**: Ombeni pamoja ili watoto na vijana wenu wawe na ujasiri wa kusema kwa ujasiri na kuishi kwa Mungu kwa njia anazowaongoza, bila kujali mapungufu yoyote yanayoonekana. Omba kwamba kanisa lako liwe jamii inayowakubali vijana na kutoa nafasi kwa sauti zao kusikika. Mshukuru Mungu kwa mahali ambapo tayari hili linatokea na mahali ambapo Mungu anafanya kazi katika maisha ya vijana wako. Omba kwamba Mungu akufunulie jinsi unavyoweza kusaidia zaidi 'kusikia' kwa vijana katika familia ya kanisa lako kwenda mbele.*

KUONEKANA NA KUSIKIKA

Siku ya Kimataifa ya Maombi ya Watoto na Vijana

# UTAFITI WA MIPANGO YA IBADA

**Ungependa tuimbe wimbo gani wa kuabudu kama sehemu ya ibada?**

**Je! Kuna michezo / shughuli zozote unazofikiria tunapaswa kujumuisha?**

**Unafikiri watu wanapaswa kuomba juu ya masuala gani yanayohusiana na watoto au vijana kama sehemu ya ibada?**

**Je! unaweza kutumia karama na talanta zako kwa njia yoyote ile unayoweza ili kuchangia / kushiriki ibada?**

**Je! Unafikiri ni kitu gani kingine kinapaswa kuongezwa / kujumuishwa katika ibada?**